**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS- TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO**

Simu; 028-2982515/0754 884134
Chatosecondaryschool@yahoo.com

**SHULE YA SEKONDARI CHATO,**
S. L .P 102,
CHATO.

**Tarehe…………….**

**Kumb.Na.CSS/ADM/F.V/2018/2019**

**MZAZI/MLEZI WA**____________________________

__________________________________________

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI CHATO MWAKA 2018/2019 MCHEPUO WA CBG ☐ HGL ☐**

Ninayo furaha kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule ya sekondari Chato. **HONGERA SANA NA KARIBU SANA.**

**1. MAHALI SHULE ILIPO**

Shule ya sekondari Chato ipo mkoani Geita wilaya ya Chato umbali wa kilometa tatu kutoka stendi kuu ya mabasi jirani na hospitali ya wilaya ya Chato na kituo cha polisi Chato.

**NAMNA YA KUSAFIRI KUFIKA CHATO.**

- Kwa wanaotoka mkoa wa Kigoma,wapande magari ya kwenda Mwanza ,wateremkie Bwanga au Buseresere na hapo wapande magari ya kwenda Mganza/Chato wateremkie Chato.
- Wanaotoka mkoa wa Kagera wilaya za;Bukoba,Karagwe,Muleba wapande magari ya kwenda Mwanza wateremkie Chato.Wanaotoka wilaya za Ngara na Biharamulo wapande magari ya kuja Chato.
- Kwa wanaotoka mikoa ya Mara,Arusha,Simiyu,Dododo,Singida,Manyara,Kilimanjaro,Dar es salaam,wapande magari yanayokwenda Mwanza,wakifika Mwanza wapande magari yaendayo Bukoba wateremkie Chato.

**2. SHERIA ZA SHULE**

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na.25 ya mwaka 1978, pia inazingatia miongzo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini.

Hivyo kwa kipindi chote utakapokuwa mwanafunzi wa shule hii,utatakiwa kushika na kuheshimu sheria,kanuni na taratibu zote za shule ukiwa ndani na nje ya shule **kwani utakuwa ukiiwakilisha shule popote utakapokuwa. Kutokujua sheria hakutakuwa kinga ya kutokuchukuliwa hatua stahiki**.

**3. SARE YA SHULE**

Wakati wote wa muda wa masmo mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare ya shule ambayo ni suruali nyeusi na shati nyeupe (mikono mirefu) na suruali nyeusi na T-sheti ya shule baada ya muda wa masomo , siku za sikukuu pamoja na Jumamosi na Jumapili

**Kwa sababu yoyote ile mwanafunzi haruhusiwi kumiliki au kuvaa nguo za kiraia (asije nazo kabisa).**

Pamoja na barua hii naambatisha viambatisho vifuatavyo. (a) Orodha ya maitaji,(b) Mchanganuo wa malipo.(c)sheria za shule,(d) Fomu ya kukubali ,(e)Fomu ya taarifa binafsi ya mwanafunzi,(f) Fomu ya mzazi/mlezi na (g )Fomu ya hospitali.

**4.KUFUNGUA SHULE**

Mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **1/7/2018** na mwisho wa kuripoti ni tarehe 15/7/2018

**ANGALIZO; Shule haipokei fedha taslimu kiwango chochote. Malipo yote yafanyike tawi lolote la benki ya NMB kupitia akaunti za shule zilizotolewa katika kiambatisho (b).**

…………….....
**SELEMA M. BERNARDO**
**MKUU WA SHULE**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO**
**SHULE YA SEKONDARI CHATO**

**MAHITAJI**

**(a) Vifaa**

- ✓ Suruali mbili nyeusi za kushona **zisizobana mwili (modal)** zenye malinda 4 na 'turn up'
- ✓ Mashati meupe mawili ya mikono mirefu.
- ✓ Tai nyeusi
- ✓ Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba visivyo na visigino virefu.
- ✓ Mkanda mweusi wa suruali usio na chuma kikubwa au chenye maandishi.
- ✓ Soksi jozi mbili rangi yoyote.
- ✓ Sweta rangi ya bluu yenye nembo ya shule (inapatikana shuleni )
- ✓ T-shirt mbili zenye nembo ya shule (zinapatikana shuleni)
- ✓ Godoro imara futi 2 ½ kwa futi 6
- ✓ Shuka 'pair' 2 rangi ya bluu kwa ajili ya kutandika na kujifunika.
- ✓ Chandarua ya duara 4/6 na foronya/mto .
- ✓ Ndoo mbili lita 10 kwa ajili ya kuchotea maji ya kuoga na mtumizi mengine.
- ✓ Sahani,bakuli,kikombe,na kijiko kwa ajili ya chakula.
- ✓ Kandambili kwa ajili ya kuogea **tu**.
- ✓ Raba jozi moja kwa ajili ya michezo.
- ✓ Mguo za michezo **Track suit rangi ya kijani kibichi**
- ✓ Ufagio wa plastiki wa dukani (soft/ broom),ufagio wa chelewa wenye mpini kwa ajili ya usafi wa nje , raba (mopper) kwa ajili kudekia,jembe,ndoo na kwanja.
- ✓ Ream moja ya karatasi nyeupe A4 (kila mwaka).
- ✓ Shajala moja (file) kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu za mwanafunzi.
- ✓ Nakala ya cheti cha kuzaliwa/uraia (siyo kadi ya kliniki).
- ✓ Hati maalum ya vipimo kutoka kwa daktari kuthibitisha afya yako.
- ✓ Nakala ya taarifa ya matokeo kidato iv (result slip)
- ✓ Kikokotozi (scientific calculator) na Dissecting kit kwa waliochaguliwa mchepuo wa CBG na Advanced Learner's Dictionary kwa mchepuo wa HGL ni lazima.
- ✓ Madaftari makubwa saba (counter book 4quires) na madaftari madogo saba

## (b) Malipo

- ✓ Fedha ya walinzi,wapishi na vibarua wengine Tsh 30,000/=
- ✓ Nembo ya shule Tsh. 2,000/=
- ✓ Fedha ya ukarabati wa samani Tsh 15,000/=
- ✓ Fedha ya taaluma Tsh. 20,000/=
- ✓ Fedha ya matibabu Tsh. 10,000/=
- ✓ Karo Tsh. 70,000/= kwa mwaka (35,000 kwa muhula)
- ✓ Fedha ya picha na kitambulisho Tsh. 6,000/=
- ✓ Fedha ya tahadhari Tsh. 5000/=
- ✓ Fedha ya maji Tsh.10,000/=
- ✓ Fedha ya umeme Tsh.10,000/=
- ✓ Uendeshaji mitihani ya kujipima Tsh.10,000/=

*Kiambatisho (b)*

# MCHANGANUO WA MALIPO NA VIFAA

**1.** Michango ifuatayo iwekwe kaika akaunti ya shule inayoitwa "CHATO SECONDARY SCHOOL RECCURENT ACCOUNT" Na. **32701200036 NMB** :

| NA. | AINA YA MCHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| 1. | Karo (kwa mwaka) unaweza kulipa nusu muhula wa 1 | 70,000/= |
| 2. | Taaluma (kwa mwaka)unaweza kulipa nusu muhula wa 1 | 20,000/= |
| 3. | Walinzi,Wapishi na vibarua wengine (15000/= kwa muhula) | 30,000/= |
| 4. | Tahadhari (mara moja) na haitarejeshwa | 5,000/ |
| 5. | Umeme (unaweza kulipa nusu muhula wa 1) | 10,000/= |
| **JUMLA** | | **135,000/=** |

<u>**2.** Michango mingine iwekwe katika akaunti ya shule inayoitwa CHATO SEKONDARI ELIMU YA KUJITEGEMEA Na.**32702300005 NMB**</u>

| NA. | AINA YA MCHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| 1. | Ukarabati wa samani (maramoja) | 15,000/= |
| 2. | Matibabu (kwa mwaka) unaweza kulipa ½ kwa muhula | 10,000/= |
| 3. | Nembo ya shule 2000/= | 2000/= |
| 5. | Kitambulisho na picha (mara moja) | 6000/= |
| **6** | Maji (unaweza kulipa ½ kwa) | 10,000/= |
| 7. | Uendeshaji mitihani ya kujipima | 10,000/= |
| **JUMLA** | | **53,000/=** |

**3. Vifaa vya kuleta shuleni ni hivi vifuatavyo**:

| NA | AINA YA KIFAA | IDADI |
|---|---|---|
| 1. | Ream 1 ya karatasi A4 (kila mwaka) | 01 |
| 2. | Ufagio wa dukani au reki | 01 |
| 3. | Jembe | 01 |
| 4. | Kwanja | 01 |
| 5. | Ndoo ndogo lita 10 | 02 |
| 6. | Shajala (file) | 01 |
| 7. | Raba(Mopper) kwa ajili ya kudekia | 01 |

***Mzazi/mlezi unasisitizwa kukamilisha michango kwa wakati ili kuepuka usumbufu.Kwa ufafanuzi endapo utapata utata piga Na.0756640199 au namba iliyotolewa katika barua ya kujiunga.***

**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO**
**SHULE YA SEKONDARI CHATO**

# SHERIA ZA SHULE

**(a) TARATIBU NA KANUNI ZA SHULE**

1.**HESHIMA**:Kila mwanafunzi anatakiwa kwanza kujiheshimu mwenyewe, kuwaheshimu walimu,wazazi/walezi,wageni na viongozi kwa ujumla.
2**. MAWASILIANO**:Kingereza ndiyo lugha pekee ya mawasiliano hapa shuleni,hivyo mwanafunzi haruhusuwi kuasilina kwa lugha nyingine yoyote isipokuwa tu wakati wa midaharo ya Kiswahili.
3.**USAFI**:Kila mwanafunzi anatakiwa kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule kwa ujumla.

4.**RATIBA YA SHULE**: Kila mwanafunzi anapaswa kuheshimu ratiba ya shule.Mwanafunzi haruhusiwi kuwa nje ya mazingira ya shule bila ruhusa maalum kutoka kwa uongozi wa shule. Aidha mwanafunzi anatakiwa kuwahi darasani na katika shughuli mbalimbali za shule ikiwa ni pamoja na kutii **kengere.**

**(b) MAKOSA YA KUMFUKUZISHA MWANAFUNZI**.
1. Wizi wa aina yoyote.
2.Uasherati, ushoga na ubakaji
3. ulevi wa pombe/madawa ya kulevya kama vile mirungi,kuber,bangi n.k
4. Kupiga/kupigana/kutoa lugha chafu kwa wanafunzi/walimu/jamii
5.Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
6.Kudharau bendera ya Taifa
7. Kuoa/kumpa mimba msichana
8.Kugoma,kuchochea/kuongoza mgomo na kuvuruga amani na usalama shuleni /jamii
9.**Mwanafunzi kumiliki line/simu ya mkononi**
10.Udanganyifu wa aina yoyote katika mitihani
11.Kugomea adhabu yoyote halali
12.Kutotii serikali iliyopo madarakani na chama tawala
13. Kuwa nje ya shule bila sare ya shule na bila ruhusa/kibali maalum kutoka kwa uongozi wa shule
14.Kuonekana kwenye nyumba za wageni na kumbi za starehe
15.Utoro/kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku tisini bila taarifa

**ANGALIZO:** Mwanafunzi atakayebainika/kukamatwa na simu atatozwa faini ya shilingi laki mbili tu (Tsh.200,000/=) Hivyo mzazi hakikisha mwanao hamiliki simu kwa namna yoyote ile ili Kuepuka kuisababishia familia hasara isiyo ya lazima.

**(c) MAKOSA YAFUATAYO YAKIJIRUDIA YATASABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**
1.Utoro wa aina yoyote ile
2.Kuchelewa kufika shuleni (baada ya likizo) na katika shughuli mbalimbali za shule.
3. Kutokuvaa sare rasmi ya shule kulingana na ratiba ya shule
4. Uchafu wa mwili (kutokunyoa ndevu/nywele,kutokuoga n.k ) na kutokutunza mazingira ya shule

**TANBIHI**: Mwanafunzi harusiwi kumiliki vifaa vya umeme kama vile simu, pasi,heater,n.k. Aidha mwanafunzi harusiwi kumiliki redio yenye kubeba memory card/frash**. Kwa kuwa mwanafunzi harusiwi kumiliki line/simu, shule itaweka utaratibu kwa wazazi/walezi kuwatumia watoto wao fedha ya matumizi kupitia simu 0754884134/ 0755392067/ 0756640199.**

*Kiambatisho(d)*

**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO**

**SHULE YA SEKONDARI CHATO,**
**S.L.P 102,**
**CHATO.**
**24 MEI,2018**

**KUMB.NA.CSS/ADM/FV/2018**

**FOMU YA KUKUBALI**

Mzazi/Mlezi wa (Jina la mwanafunzi)

______________________________

Mimi……………………………………(mwanafunzi) bila shuruti nakubali kutumia nafasi niliyopewa ya kidato cha …………….katika shule ya sekondari Chato. Pia naahidi kutokushiriki kwa namna yoyote ile katika migomo na maanadamano yasiyoruhusiwa.

……………………… ……………
Saini ya mwanafunzi tarehe

Mimi…………………………………………… mzazi /milezi wa……………………………. (mwanafunzi) nimeyasoma masharti yote ya mwanangu ya kujiunga na shule ya sekondari chato na ninakubali na kuahidi kwamba mtoto wangu atafuata masharti yote ya shule ikiwa ni pamoja na kutokushiriki kwa namna yoyote katika migomo .Aidha nitahakikisha kuwa mwanangu anamaliza elimu ya kidato cha sita kwa kuwajibika kulipa michango ya shule pamoja na maelekezo megine yatakayokuwa yakitolewa na shule.

………………………….. ………………
Saini ya mzazi/Mlezi tarehe

*Kiambatisho (e)*

**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO**

**SHULE YA SEKONDARI CHATO**

**MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

***FOMU HII IJAZWE NA MWANAFUNZI***

1. Jina kamili …………………………………………………………………………………………………………………………

2. (a)Tarehe ya kuzaliwa……………………………………………………………………………………………………………

   (b)Mahali alipozaliwa……………………………………………………………………………………………………………..

3.(a) Dini…………………………………………………………………………………………………………………………………

   (b) Dhehebu…………………………………………………………………………………………………………………………..

4. (a) Uraia……………………………………………………………………………………………………………………………..

   (b) Kama siyo raia wa Tanzania taja uraia wako………………………………………………………………………….

5. Shule ya sekondari uliyotoka…………………………………………………………………………………………………….

6. (a) Jina kamili la mzazi /mlezi………………………………………………………………………………………………..

   (b) Anwani ya mzazi/mlezi……………………………………………………………………………………………………

   (c) Kazi ya mzazi/mlezi…………………………………………………………………………………………………………….

   (d) Kituo chake cha kazi…………………………………………………………………………………………………………

   (e) Namba ya simu…………………………………………………………………………………………………………………

7. (a) Mahalia anapoishi……………………………………………………………………………………………………………..

   (b) Jina la mwenyekiti wa kitongoji/mtaa……………………………………………………………………………………..

8. (a) Je, unaishi na nani? Taja jina kamili ……………………………………………………………………………………….

   (b) Je,una uhusihano gani na huyu uliyemtaja?........................................................................

9.Ni yatima/si yatima………………………………………………………………………………...........................

10. Kama ni yatima mzazi yupi aliyefariki:mama/baba/wote……………………………………………………………………….

# CHATO DISTRICT COUNCIL

CHATO SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 102,
CHATO.
Date……………………………..

**PART 'A'**

## MEDICAL EXAMINATION FORM

STUDENT'S FULL NAME…………………………………………………………………………
TO MEDICAL OFFICER IN CHARGE OF
……………………………………………………………..
………………………………………………………………

Please examine the above named student as to his physical/mental fitness/unfitness for admission as full time student of Chato secondary school for academic year 2018/2019.

The examination should include the following categories: Eye sight, Hearing, Epilepsy, Urine, Venereal disease, Stool and any other body deformation.

…………………
THE HEADMASTER

**PART 'B' (MEDICAL EXAMINATION RESULTS)**

THE HEADMASTER,
CHATO SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 102,
**CHATO.**

I have examined the above student and found him with the following disease/ impairment/disabilities:

Eye sight……………………………………………………………………………………………
Urine examination…………………………………………………………………………………
Hearing………………………………………………………………………………………………
Stool examination…………………………………………………………………………………
Speech ……………………………………………………………………………………………..
Venereal diseases…………………………………………………………………………………
Limbs…………………………………………………………………………………………………
Epilepsy………………………………………………………………………………………………
Additional information/other serious diseases………………………………………………..
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
Name and signature of attending officer…………..…………………Date…………………………….
Designation………………………………. Official stamp………………………………………..